

Mungu Ana Maadui?

Kama mhubiri wa neno la Mungu, nawajibika kuhubiri mausia yote ya Mungu, 1 Petro 4:11. Sina haki ya kuchagua masomo yaliyo kama peremende ya pamba, na kuyafundisha hayo peke yake tena na tena, Waebrania 6:1-3. Ikiwa ninampenda Mungu, na hadhira yangu, basi nitakufundisha Neno lote la Mungu, kwa ujasiri, bila hofu, na kwa upendo, Waefeso 6:19-20; 4:15.

Kama mhubiri ninalo jukumu la kuyapinga mafundisho potofu, Yuda 1:3; Wagalatia 1:6-10, ambayo yatang'olewa na Baba (Mathayo 15:13). Na kama hadhira, unatakiwa kuyapima yanayofundishwa, ili kuhakiki kama ni mafundisho ya Mungu, 1 Yohana 4:1. Na kama ndiyo, basi tii!

Hivi karibuni nilisikia mtu akisema eti kanisa halina maadui. Maudhui ya maelezo hayo yalikuwa ni kudai kwamba kwa kuwa kanisa halina maadui, basi Mungu anawapenda wote, na tunakupokea kama ulivyo. Ndiyo, nitakubali, Biblia inafundisha kwamba Mungu anawapenda wote, Yohana 3:16. Pia, Biblia inafundisha kuwa mtu yeyote anaweza kumjia Kristo na kuzitubia dhambi zake, na kupata ondoleo la dhambi, Matendo ya Mitume 2:38; 22:16. Lakini, hivi, Biblia inafundisha kuwa kanisa halina maadui, na kufikia hatua ya kuona kuwa hata Mungu hana maadui? (1wakorintho 15:9; 2 Wakorintho 1:1)

Katika Isaya 1:24 Biblia inatanabaisha kuwa siyo tu kwamba Mungu ana wapinzani, bali pia **maadui**, na kwamba atawaadhibu kwa sababu ya maasi yao. Katika maudhui ya Isaya 1:21-31, Mungu anaongelea maadui, pia anaainisha maadui ni wepi;

Kwa mujibu Isaya 1, adui za Mungu ni akina nani?

Wazinzi wa kiroho mst 21.

Wauaji, mst 21

Wale wanaofifia kiroho, mst 22

Wakuu wadhalimu, mst 23

Wezi, mst 23

Wapendao rushwa, mst 23

Wale wasiowatetea yatima na wajane, mst 23.

Mungu atawafanyaje maadui hawa? “Nami nitakuelekezea wewe mkono wangu,” 1:25.

Ndugu, tusiendekeze injili ya peremende ya pamba kwamba Mungu anapendezwa na watu wote na kwamba hana maadui. Yakobo 4:4 yafundisha wazi wazi “kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu”

Kwa hiyo, kwa kuwa Mungu ana maadui, ndivyo na kanisa!

Fundisho la “wewe, katika dhambi, siyo adui wa Mungu,” linamfanyaje mwanadamu?

- 1) Endapo unasikiliza, huwi adui, basi hili humaanisha kuwa una amani. Hakuna sababu ya kurekebisha chochote kwa kuwa HAKUNA KOSA LOLOTE. Hivyo mtu aishiye katika dhambi kumwelezea kwamba siyo adui, hitimisho la jambo hilo ni kwamba huyo mtu yu katika amani. Yesu alifundisha kuwa kila mtu huangukia kwenye fungu moja au mawili: Kondoo au Mbuzi (Mathayo 25:31) Hivyo, kama mhubiri ananyanyuka na kusema “uliye katika dhambi wewe siyo mbuzi” hitimisho lake ni nini?
- 2) Ndugu, tunatakiwa kufundisha kwa upendo, kwamba kila aliye katika dhambi ni adui wa Mungu. Na kwa kufanya hivyo, Watu wenye mioyo iliyopondeka, wanyenyekevu watatak kufahamu cha kufanya ili kurekebisha hali. Nakumbuka huduma ya Yohana Mbatizaji (Mathayo 3:1-12). Na nabii huyu aliyetabiriwa na Mungu karne kadhaa kabla ya ujio wake (Isaya 40; Malaki 4:5; Luke 1:17), naye alifundisha nini? Je, alifundisha kuwa kila mtu aishiye katika dhambi si adui wa Mungu? Au Je, katika roho ya Eliya, akahubiri, “Tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia?” Ndipo wanyenyekevu wakaitambua dhambi, nao wakatii. Nao wenye mioyo migumu, walioamini kuwa hawana dhambi, wakakataa.

Mungu ana maadui, Kanisa lina maadui, hivyo njooni tudadisi na tuihubiri kweli iwezayo kuwatakasa watu (Yohana 17:17), badala ya kuwaambia watu ambao wako katika dhambi siyo maadui wa Mungu. Ndugu zangu huo ni uongo wa wazi wazi!

Na kabla sijamalizia, natoa onyo kwa walioijua kweli hapo kwanza, lakini sasa: wanahubiri injili nyingine

Katika waebrania 10:31, mwandishi anaandika “Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai” Hili ni kweli kwa wasioamini (maadui) na hasa hasa kwa wale waliokuwa wakristo, lakini mara wakaanguka (maadui), 2 Pet. 2:20. Kama Mungu hana maadui, kwa nini ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono yake? Kwa nini basi, 2 Petro 2:20 inatufundisha kwamba “hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza” ikizungumzia wale walionaswa tena na ulimwengu. Lihubiri Neno (2 Timotheo 4:1-4), “yakumbukeni maneno yaliyonenwa zamani na mitume wa Bwana wetu Yesu Kristo,” Yuda 1:17